TANGAZO LA SERIKALI NA. 701 la tarehe 22/9/2023

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,
(SURA YA 414)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 19)*

NOTISI YA UCHUNGUZI WA MAOMBI YA BEI ZA MAJI YA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA BIHARAMULO YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uchunguzi wa Maombi ya Bei za Maji ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Biharamulo ya Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa na Sheria ya Mamlaka na Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka; na

"uchunguzi" maana yake ni mchakato mzima wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu marekebisho ya bei yanayopendekezwa kama inavyooneshwa kwenye Majedwali ya Kwanza, Pili na Tatu ya Notisi hii.

Madhumuni ya uchunguzi

3. Madhumuni ya uchunguzi ni kuiwezesha Mamlaka kukusanya maoni ya wadau kuhusu bei zinazopendekezwa.

Mapendekezo ya bei

4. Bei zinazopendekezwa na Biharamulo WSSA zimeainishwa kwenye Majedwali ya Kwanza, Pili na Tatu ya Notisi hii.

Jinsi ya kushiriki katika uchunguzi

5. Mtu anayetaka kushiriki kwenye uchunguzi anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyotajwa katika aya ya 8 ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Pingamizi

6. Mtu anayekusudia kupinga uidhinishwaji wa maombi ya bei atawasilisha pingamizi lake kwa maandishi ndani ya siku tano za kazi kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Nakala za maombi

7. (1) Nakala za maombi ya bei ya Biharamulo WSSA zinapatikana kwenye ofisi za Mamlaka saa za kazi kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kwa ajili ya taarifa kwa umma.

(2) Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa kuwasilisha maombi kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyotajwa kwenye aya ya 8.

Anwani ya Mamlaka

8. Anwani ya Mamlaka itakuwa-
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,
Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104, Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma.
Barua Pepe: info@ewura.go.tz

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Maelezo ya Aina ya Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2024/26 |
| Majumbani 1-5 | 1350 | 1650 | 1850 | 2, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Majumbani 6-10 | 1420 | 1750 | 1950 | 2 |
| Majumbani >11 | 1440 | 1890 | 1990 | 2 |
| Taasisi | 1700 | 1900 | 2000 | 2 |
| Biashara | 1730 | 1990 | 2300 | 2 |
| Viwanda | 2000 | 2200 | 2,500 | 2, |
| Waosha Magari | | 2590 | 3100 | 3 |
| Magati | 1500 | 1500 | 1600 | 1 |
| **Wastani wa Bei** | **1591** | **1934** | **2161** | **2** |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho ya Huduma (Shilingi kwa Unganisho)

| Maelezo ya Aina ya Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoainiswa katika kanuni 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |
| Magati | | | | |
| Wateja Wakubwa | | | | |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi kwa Rejesho)

| Maelezo ya Aina ya Wateja | Ada za Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/2023 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 15.000 | 18,00 | 20,00 | 20,00 |
| Taasisi | 15,000 | 22,00 | 25,00 | 30,00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Biashara | 15,000 | 22,00 | 25,00 | 30,00 |
| Viwanda | 15,000 | 22,00 | 30,00 | 30,00 |
| Waosha Magari | 15,000 | 22,00 | 30,00 | 30,00 |
| Magati | 15,000 | 22,00 | 25,00 | 25,00 |

Dodoma,                                                  JAMES A. MWAINYEKULE

.........................., 2023                                  *Mkurugenzi Mkuu*